BODI YA KOROSHO TANZANIA

MWONGOZO WA UZALISHAJI MICHE NA UPANDAJI MIKOROSHO BORA 10,000,000 KWA MSIMU WA 2017/2018

UMETOLEWA CHINI YA SHERIA YA TASNIA YA KOROSHO NA. 18 YA MWAKA 2009 NA KANUNI ZAKE ZA MWAKA 2010, KANUNI YA 59

Umeandaliwa na:

Bodi ya Korosho Tanzania,
S.L.P 533,
Mtwara, Tanzania.

DESEMBA, 2017

TAFSIRI YA MAANA YA MANENO YALIYOTUMIKA

Katika mwongozo huu, maneno yafuatayo yanatafsiriwa kama ifuatavyo:-

“Sheria” maana yake ni sheria ya Tasnia ya korosho Na. 18 ya mwaka 2009

“CBT” (*Cashew nut Board of Tanzania*) maana yake ni Bodi ya Korosho Tanzania

“NARI” (*Naliendele Agricultural Reasearch Institute)* maana yake ni Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Naliendele

“CDC” (*Cashew Development Centre)* maana yake ni Vituo vya Uendelezaji Zao la Korosho

“DSMS-Cashew” (*District Subject Matter Specialist-Cashew*) maana yake ni Waratibu wa zao la korosho katika Halmashauri ya Wilaya/Mji/Manispaa/Jiji

“WEO” (*Ward Executive Officer*) maana yake ni Afisa Mtendaji wa Kata

“VEO” (*Village Executive Officer*) maana yake ni Afisa Mtendaji wa Kijiji

“WAEO” (*Ward Agriculture Extension Officer*) maana yake ni Afisa Ugani wa Kata

“VAEO” (*Village Agriculture Extension Officer*) maana yake ni Afisa Ugani wa Kijiji

SEHEMU YA KWANZA

1.0 UTANGULIZI

Bodi ya Korosho Tanzania (CBT), kwa kushirikiana na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Naliendele, Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri, imeandaa Mpango wa miaka mitatu (3) wa uzalishaji miche na upandaji mikorosho mipya (2016/2017 hadi 2018/2019). Katika mpango huu inatarajiwa kupandwa wastani wa mikorosho 5,000 kila kijiji au mikorosho 30 kwa kaya kwa mwaka, sawa na mikorosho 10,000,000 au ekari 330,000 kwa mwaka kwa nchi nzima. Katika mwaka 2017/2018 mpango huu utajumuisha Halmashauri za wilaya 90 katika mikoa 17 (Kiambatisho Na. 1), iliyothibitishwa kustawi zao la korosho hapa nchini. Lengo ni kuinua kipato cha mkulima kwa kuongeza uzalishaji, ubora na tija katika kilimo cha zao la korosho.

Mwongozo huu unatoa utaratibu wa upatikanaji wa vifaa na mbegu za kuzalisha miche, sifa za eneo la uzalishaji na mzalishaji, ugawaji wa miche, malipo ya wazalishaji miche na majukumu ya kila mdau katika utekelezaji wa mpango.

SEHEMU YA PILI

2.0 MAJUKUMU YA WADAU KATIKA UTEKELEZAJI WA MPANGO

Majukumu ya wadau katika kutekeleza mpango huu kitaifa ni kama yalivyoainishwa hapa chini.

2.1. Bodi ya Korosho Tanzania

Majukumu ya Bodi ya Korosho katika utekelezaji wa mpango ni kama yafuatayo:-

(i) Kupokea taarifa za mahitaji, uzalishaji miche na upandaji mikorosho kutoka Halmashauri na kuziainisha (analyse) kwa lengo la kutoa maelekezo kuhakikisha malengo ya mpango yanatimia

(ii) Ununuzi wa vifaa vya vitalu vya mikorosho kama vile matandazo, viriba vyeusi, viriba vyeupe na vivuli wavu (shade net).

(iii) Ununuzi wa mbegu bora kutoka NARI

(iv) Ununuzi wa miche bora ya mikorosho

(v) Usambazaji wa mbegu na vifaa kwa halmashauri husika.

(vi) Kuingia mikataba na Wazalishaji miche juu ya uzalishaji wa miche bora ya mikorosho

(vii) Kufanya usisimamizi/ufuatiliaji na tathmini ya mpango

(viii) Kutunza taarifa za uzalishaji na usambazaji wa miche na mikorosho

2.2 Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Naliendele (NARI)

Majukumu ya NARI katika utekelezaji wa mpango ni kama ifuatavyo:-

(i) Kuzalisha mbegu bora za korosho na kukabidhi kwa Bodi ya Korosho Tanzania kwa kufuata kalenda ya mwaka ya uzalishaji husika.

(ii) Kuzalisha vikonyo kwa ajili ya kubebeshea kwenye miche ya korosho

(iii) Kutoa elimu kwa Maafisa ugani, wakulima, viongozi na wazalishaji miche juu ya uanzishaji wa vitalu na mbinu bora za kilimo cha korosho.

(iv) Kufanya tathmini ya maeneo yanayofaa kwa kilimo cha zao la korosho Kuhakiki ubora wa miche inayozalishwa

2.3 Halmashauri ya Mji/Wilaya/Manispaa/Jiji

Majukumu ya Halmashauri katika utekelezaji wa mpango ni kama yafuatayo:-

(i) Kupokea mahitaji ya miche kutoka kwa watendaji wa vijiji/mkulima na kuwasilisha Bodi ya Korosho

(ii) Kuteua vikundi vya uzalishaji miche

(iii) Kutoa taarifa/takwimu za mashamba yaliyoanzishwa na yaliyotelekezwa na kupendekeza mashamba ya kujumuishwa kwenye mpango kwa msimu husika

(iv) Kuwasilisha Bodi ya Korosho, taarifa ya maendeleo ya utekelezaji wa mpango.

(v) Kutoa mafunzo ya uanzishaji wa mashamba mapya na ufufuaji wa mashamba yaliyotelekezwa.

(vi) Kusimamia na kufuatilia wakati wa utekelezaji na baada ya mpango kumalizika

(vii) Kutenga na kutumia sehemu ya fedha kwenye bajeti za Halmashauri kwa ajili ya kutekeleza mpango wa upandaji mikorosho mipya.

(viii) Kutunga na kusimamia sheria ndogondogo (by laws) kwa ajili ya kuhakikisha wakulima wanapanda na kuihudumia mikorosho iliyogawiwa.

2.4 Waratibu wa zao la korosho (DSMS-Cashew)

(i) Kuratibu na kusimamia uanzishwaji wa vitalu vya miche, usambazaji na upandaji miche na mbegu bora kwa wakulima

(ii) Kuwasilisha Bodi ya Korosho, taarifa za maendeleo ya uzalishaji miche kila mwezi

(iii) Kuwasilisha Bodi ya Korosho taarifa ya mikorosho iliyopandwa kwa kila mkulima, miche iliyofanikiwa kukua na miche iliyokufa.

2.5 Sekta Binafsi hususani vikundi vya Uzalishaji Miche.

Majukumu ya vikundi vya uzalishaji miche ni kama ifuatavyo

(i) Kuingia mikataba na Bodi ya Korosho Tanzania ya uzalishaji na usambazaji wa miche bora ya mikorosho

(ii) Kuzalisha miche kwa kutumia mbegu bora zilizozalishwa na NARI

(iii) Kuzalisha miche kwa kufuata mwongozo wa utunzaji wa kitalu na ubebeshaji wa mikorosho uliotolewa na Bodi ya Korosho

(iv) Kuwasilisha madai ya uzalishaji wa miche Bodi ya Korosho yakiambatana na fomu ya ugawaji miche ya mikorosho ikiwa na; majina ya wakulima, idadi ya miche ya mikorosho waliochukua, namba za simu na saini za wakulima waliopokea miche hiyo.

(v) Awe tayari kupokea malipo yake kupitia benki na kuwasilisha stakabadhi ya Malipo Bodi ya Korosho Tanzania.

2.6 Mkulima

Majukumu ya wakulima katika utekelezaji wa mpango ni kama yafuatayo:-

(i) Kuandaa Mashamba kwa wakati

(ii) Kuwasilisha mahitaji ya miche/mbegu kwa watendaji wa vijiji

(iii) Kufuata na kupokea miche/mbegu kutoka katika kitalu kilichokaribu

(iv) Kupanda miche kwa kufuata maelekezo ya wataalamu wa kilimo.

(v) Kuhudumia miche na kuhakikisha inakua vizuri

(vi) Kutoa taarifa kwa Mtaalamu wa Kilimo (VEOs, VAEOs) endapo mche utakufa na sababu zake

(vii) Kujisajili katika fomu maalum itakayotolewa na CBT kabla ya kupokea miche

2.7 Viongozi na Watendaji ngazi ya kijiji na Kata (WEOs, VEOs, WAEOs NA VAEOs)

Majukumu ya viongozi na Watendaji katika ngazi za Vijiji na Kata ni kama ifuatavyo:-

(i) Kutenga maeneo ya kilimo cha korosho kutoka kwenye ardhi ya kijiji/vijiji.

(ii) Kupokea mahitaji ya miche kutoka kwa mkulima na kuwasilisha katika Halmashauri husika

(iii) Kuhamasisha na kusimamia utayarishaji wa mashamba mapya na ufufufaji wa mashamba yaliyotelekezwa.

(iv) Kuhakikisha kuwa mashamba yaliyoanzishwa na yaliyofufuliwa yanakuwa endelevu

(v) Kuwasilisha taarifa ya maendeleo ya utekelezaji wa mpango kwenye Halmashauri

(vi) Kusimamia sheria ndogondogo (by laws) zinazoundwa na Halmashauri

(vii) Kujaza fomu za taarifa ya wakulima watakaochukua miche (VEOs)

(viii) Kutoa taarifa kwa mratibu wa Zao la Korosho Wilaya kuhusu mikorosho iliyokufa, mkulima husika na sababu zake.

2.8 Ofisi ya Mkuu wa Wilaya

Majukumu ya Ofisi ya Mkuu wa Wilaya katika utekelezaji wa mpango ni kama yafuatayo:-

(i) Kuhamasisha Wakulima na viongozi ngazi ya Wilaya, Kata na vijiji kutekeleza agizo la kupanda mikorosho 5,000 kwa kila kijiji kwa mwaka.

(ii) Kusimamia Wakulima na viongozi ngazi ya Wilaya, Kata na vijiji kuainisha maeneo, kuandaa mashamba mapya na vitalu vya miche kwa kila kijiji.

(iii) Kusimamia zoezi la ugawaji miche na upandaji mikorosho katika mashamba

(iv) Kuratibu shughuli zote za utekelezaji wa mpango huu katika wilaya husika.

2.9 Ofisi ya Mkuu wa Mkoa

Majukumu ya Ofisi ya Mkuu wa Mkoa katika utekelezaji wa mpango ni kama yafuatayo:-

(i) Kuhamasisha Wakulima na viongozi ngazi ya Mkoa, Wilaya, Kata na vijiji kupokea agizo la kupanda mikorosho 5,000 kwa kila kijiji kwa mwaka.

(ii) Kusimamia Wakulima na viongozi ngazi ya Mkoa, Wilaya, Kata na vijiji kuainisha maeneo na kuandaa mashamba mapya na vitalu kwa kila kijiji.

(iii) Kuratibu shughuli zote za utekelezaji wa mpango huu katika Mkoa husika.

SEHEMU YA TATU

3.0 UTARATIBU WA UTEKELEZAJI WA MPANGO

3.1 KUCHAGUA WAZALISHAJI MICHE

Mzalishaji wa miche ni mtu binafsi au kikundi cha wakulima au Taasisi yoyote iliyoteuliwa na Halmashauri ya Wilaya kuzalisha miche isiyobebeshwa na/au iliyobebeshwa.

Ili mzalishaji aweze kuteuliwa anatakiwa awe na sifa zifuatazo:-

3.1.1 Sifa za Mzalishaji Miche

(i) Awe na eneo linalofaa kwa ajili ya kitalu cha miche ya mikorosho

(ii) Awe tayari kupewa elimu ya uzalishaji wa miche ya mikorosho, utunzaji wa kitalu na magonjwa ya mikorosho hasa michanga.

(iii) Awe tayari kusaini mkataba wa kuzalisha miche ya mikorosho na Halmashauri yake pamoja na Bodi ya Korosho Tanzania.

(iv) Awe tayari kuzalisha miche ya mikorosho, kuihudumia na kuigawa kwa wakulima kwa kufuata maelekezo ya Bodi ya Korosho kupitia Halmashauri yake.

(v) Awe na akaunti benki.

3.1.2 Uteuzi wa mzalishaji miche

Uteuzi wa mzalishaji miche unafanywa na Halmashauri ya wilaya husika baada ya kuthibitisha mzalishaji ametimiza sifa za uzalishaji miche. Idadi ya wazalishaji miche na kiasi cha uzalishaji hutegemea malengo ya Halmashauri na upatikanaji wa mbegu bora katika msimu husika.

3.1.3 Sifa za eneo linalofaa kwa kitalu cha miche ya mikorosho

(i) Eneo liwe linafikika kwa urahisi kwa ajili ya utoaji huduma kwenye kitalu kwa mfano kupeleka pembejeo, kuhamisha miche nk

(ii) Eneo liwe lenye uhakika wa upatikanaji wa maji safi yasiyokuwa na chumvi ya kumwagilia miche ya mikorosho kwa kipindi kisichopungua miezi miwili

(iii) Eneo la kitalu liwepo karibu na wahitaji ili kupunguza gharama za usafirishaji.

(iv) Eneo liwe lina udongo unaofaa kukuzia miche (udongo tifutifu/kichanga).

(v) Kitalu kiwe kwenye eneo lisilotuamisha maji

(vi) Eneo liwe halina visumbufu vya mimea na misongo ya kimazingira inayoweza kusababisha uharibifu wa miche

3.2. UPATIKANAJI WA MBEGU NA VIFAA VYA UZALISHAJI MICHE

(i) Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Naliendele itazalisha mbegu bora za korosho na zitanunuliwa na Bodi ya Korosho na kusambazwa kwa wakulima bila malipo.

(ii) Miche iliyobebeshwa ya mikorosho itazalishwa kwa kutumia vikonyo kutoka vituo vya Uendelezaji Zao la Korosho (CDCs) na mashamba ya wakulima yaliyothibitishwa na NARI kuwa na mikorosho bora.

(iii) Ununuzi wa vifaa vya uzalishaji miche na usambazaji utasimamiwa na Bodi ya Korosho Tanzania.

(iv) Mbegu pamoja na vifaa ambavyo vitagawiwa bure kwa wazalishaji ni viriba vyeusi, matandazo, viriba vyeupe na vivuli wavu (*shade net*).

(v) Kiasi cha mbegu na vifaa vitakavyogawiwa kwa kila mzalishaji kitategemea malengo ya uzalishaji yaliyokubalika.

3.3. MAFUNZO YA WAZALISHAJI MICHE

Ili kuwezesha wazalishaji wa miche kufanya kazi kwa ufanisi na kusimamia matumizi ya fedha (value for money), katika mpango huu kutakuwa na mafunzo yatakayotolewa kwa baadhi ya wagani na wawakilishi wa wazalishaji wa miche kutoka Halmashauri zote zinazolima Korosho nchini. Katika mafunzo haya mada zitakazofundishwa ni pamoja na uzalishaji wa miche, utunzaji wa kitalu, udhibiti wa wadudu na magonjwa ya mikorosho. Mafunzo hayo yatatolewa na Taasisi ya Utafiti wa kilimo Naliendele chini ya uratibu wa Bodi ya Korosho Tanzania.

3.4 UGAWAJI WA MICHE

Kabla ya ugawaji wa miche, Bodi ya Korosho Tanzania kwa kushirikiana na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Naliendele, Mratibu wa Korosho wilaya husika (DSMS-Cashew) watahakiki ubora wa miche iliyozalishwa na idadi ya miche kulingana na mkataba alioingia na Bodi. Baada ya uhakiki, mzalishaji atakabidhi miche hiyo kwa Bodi na Bodi itaikabidhi Halmashauri husika kwa ajili ya kuigawa kwa wakulima. Mratibu wa korosho (DSMS-Cashew) atasimamia ugawaji wa miche hiyo kwa wakulima na kila mkulima atajaza fomu maalum ya makabidhiano

3.5 MALIPO YA UZALISHAJI MICHE

Baada ya Bodi ya Korosho kutoa vifaa na mbegu bure na wazalishaji kuotesha miche malipo yatafanyika kwa awamu moja. Mzalishaji atalipwa asilimia mia moja (100%) ya thamani ya idadi ya miche aliyozalisha yenye ubora uliokusudiwa, iliyokubaliwa na kuikabidhi kwa Bodi ya Korosho Tanzania.

Aidha, Halmashauri na wakulima watatakiwa kulipia gharama za usambazaji wa mbegu na miche kutoka halmashauri/vitalu husika hadi sehemu zinakohitajika kupandwa.

3.7 USIMAMIZI WA MPANGO, UFUATILIAJI NA TATHMINI (M&E).

Mpango huu wa kupanda mikorosho 10,000,000 utatekelezwa kwa utaratibu wa shughuli za pamoja (shared functions) kati ya Bodi ya Korosho (CBT), NARI na Sekretarieti za mikoa. Ufuatiliaji utafanywa na CBT kwa hatua mbalimbali kuanzia uzalishaji, usafirishaji na usambazaji.

Tathmini itafanyika mwishoni mwa Mpango (*Final Project Evaluation*) na inatarajiwa kuwashirikisha kikamilifu wadau wote wa mpango na itafanywa na taasisi nyingine au wataalamu binafsi (*External Evaluator*) kwa kadri watakavyopendekezwa na Bodi ya Korosho (CBT).

SEHEMU YA NNE

4.0 MAMBO YA UJUMLA

4.1 Mwongozo huu unalenga kutoa utaratibu wa utekelezaji wa mpango wa uzalishaji miche na kupanda mikorosho mipya 30,000,000 kwa kipindi cha miaka mitatu. Maelekezo yametolewa juu ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali za mpango huu kama vile ununuzi wa mbegu, vifaa, usambazaji na ugawaji wa miche kwa wakulima. Aidha, majukumu mbalimbali ya kila

mdau yameelezwa ili kufanikisha azma ya Serikali ya kuongeza kiasi cha korosho kinachozalishwa nchini. Hivyo ni jukumu la kila mdau kuhakikisha anatimiza wajibu wake katika kuendeleza Tasnia ya Korosho nchini kwa kuzingatia mwongozo huu.

4.2 Mwongozo huu utasomwa pamoja na sheria ya Tasnia ya Korosho Na. 18 ya mwaka 2009 kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2010 na kanuni zake za mwaka 2010.

4.3 Mwongozo huu utatekelezwa na wadau wote waliotajwa kwenye mwongozo huu na endapo mtu yeyote atakiuka kutekeleza au kutenda kosa kwa mujibu wa mwongozo huu, atachukuliwa hatua za kisheria kwa mujibu wa sheria Na. 18 ya mwaka 2009 kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2010.

MWONGOZO HUU UMESAINIWA LEO TAREHE ...04/01/2018...

.....

Hassan M. Jarufu

KAIMU MKURUGENZI MKUU

HALMASHAURIZA WILAYA ZILIZO KATIKA MPANGO WA KUPANDA MIKOROSHO BORA MSIMU WA 2017/2018

MKOA		#	HALMASHAURI
1	**MTWARA**	**1**	Tandahimba dc
		2	Newala tc
		3	Newala dc
		4	Nanyamba
		5	Nanyumbu
		6	Mtwara dc
		7	Mtwara mc
		8	Masasi tc
		9	Masasi dc
2	**LINDI**	**10**	Liwale
		11	Lindi dc
		12	Nachingwea
		13	Kilwa
		14	Lindi manispaa
		15	Ruangwa
3	**PWANI**	**16**	Kibaha tc
		17	Kibaha dc
		18	Bagamoyo
		19	Chalinze
		20	Kibiti
		21	Kisarawe
		22	Mafia
		23	Mkuranga
		24	Rufiji
4	**TANGA**	**25**	Handeni dc
		26	Handeni tc
		27	Kilindi dc
		28	Korogwe dc
		29	Korogwe tc
		30	Mkinga
		31	Muheza
		32	Pangani dc
		33	Tanga cc
5	**MOROGORO**	**34**	Morogoro dc
		35	Malinyi
		36	Kilosa
		37	Ulanga
		38	Mvomero
		39	Gairo dc
		40	Mahenge/ulanga
6	**RUVUMA**	**41**	Nyasa
		42	Tunduru

		43	Mbinga tc
		44	Madaba
		45	Mbinga dc
		46	Songea dc
		47	Namtumbo
7	**MBEYA**	**48**	Kyela
		49	Chunya
		50	Mbarali
8	**IRINGA**	**51**	Iringa dc
		52	Kilolo dc
9	**DODOMA**	**53**	Mpwapwa dc
		54	Kondoa tc
		55	Kongwa dc
		56	Bahi
		57	Kondoa dc
		58	Chamwino
		59	Dodoma mc
		60	Chemba dc
10	**SINGIDA**	**61**	Mkalama
		62	Itigi
		63	Manyoni
		64	Singida mc
		65	Ikungi dc
		66	Iramba dc
11	**NJOMBE**	**67**	Ludewa
		68	Makete
12	**TABORA**	**69**	Igunga dc
		70	Kaliua dc
		71	Nzega dc
		72	Nzega tc
		73	Sikonge dc
		74	Tabora mc
		75	Urambo dc
		76	Uyui dc
13	**KILIMANJARO**	**77**	Moshi dc
		78	Same dc
		79	Mwanga dc
		80	Siha dc
		81	Hai dc
		82	Rombo dc
14	**SONGWE**	**83**	Songwe dc
		84	Ileje dc
15	**KATAVI**	**85**	Mpanda dc
		86	Mpanda mc
		87	Nsimbo dc
		88	Mlele dc
16	**KIGOMA**	**89**	Uvinza dc
17	**SHINYANGA**	**90**	Ushetu tc

BODI YA KOROSHO TANZANIA

Fomu Namba……..

FOMU YA KUPOKEA MICHE YA MIKOROSHO BORA MSIMU WA 2017/2018

(Fomu hii ijazwe na Mkulima mbele ya Afisa Mtendaji wa Kijiji anachoishi na kisha aikabidhi kwa Mzalishaji wa Miche anayopokea ambaye ataikabidhi kwa Mkurugenzi wa Halmashauri kisha kwa Mkurugenzi wa Bodi ya Korosho Tanzania)

Mkoa…….Wilaya…….Kata…….
Kijiji/Mtaa ……....Kitongoji……

A: MAELEZO BINAFSI

(i) Jina la Mkulima (Majina Matatu)……..
(ii) Jinsia……..
(iii) Umri (Miaka)…….
(iv) Aina ya Kitambulisho……..Namba…….(Kama hakuna Kitambulisho tafadhali tumia barua ya utambulisho kutoka kwa Afisa Mtendaji wa Kijiji/Kitongoji/Mtaa)
(v) Anuani ya Posta…….
(vi) Namba ya Simu……..**.....**

B: MAELEZO KUHUSU SHAMBA

(i) Mahali Shamba lilipo, Kata……Kijiji……
(ii) Ukubwa wa Shamba (Idadi ya ekari)……
(iii) Aina ya Shamba, Jipya…….La Zamani……(Tafadhali weka alama ya vema palipo na jibu sahihi).
(iv) Idadi ya Mikorosho iliyopo shambani hivi sasa ni……Kati ya hii ya Kisasa (Mikorosho Bora) ni……..na Mikorosho ya Asili (Kienyeji) ni……..
(v) Idadi ya mashimo yaliyoandaliwa kwa ajili ya kupanda mikorosho bora msimu huu ni…….

C: MAELEZO KUHUSU MICHE

(i) Tarehe inayopokelewa miche……../……...../20……
(ii) Jina la Mzalishaji Miche……
(iii) Mahali Miche inapopokelewa……..
(iv) Idadi ya Miche inayopokelewa, Isiyobebeshwa…….Iliyobebeshwa……Jumla…….

D: MAKABIDHIANO

Makabidhiano haya yamefanyika leo tarehe…….

Kati ya Mzalishaji Miche Bw./Bi/Kikundi……..**.....**Saini……

NA

Mkulima Bw./Bi…….Saini …….

MBELE YA

Afisa Mtendaji wa Kijiji cha……Bw./Bi……

Saini na kitambulisho ……..**.....**

NA KUTHIBITISHWA NA

Mkurugenzi Mtendaji (W) Wilaya ya …… Bw./Bi…….**.....**…….

Saini na muhuri……..…….**.....**

NB: Fomu hii ijazwe katika nakala nne (4)

BODI YA KOROSHO TANZANIA – (CBT)

TAARIFA YA UGAWAJI WA MICHE YA MIKOROSHO BORA MSIMU WA .....

(Fomu hii ijazwe na Msambazaji wa miche kwa ukamilifu na kuirejesha kwa Mkurugenzi Mkuu - Bodi ya Korosho Tanzania P.O. Box 533 Mtwara).Mkoa_____Wilaya _____Kata_____ Kijiji _____

NA.	JINA LA MKULIMA	UMRI	KE/ME	KIJIJI ANACHOTOKA	IDADI YA MICHE		NAMBA YA SIMU	SAINI YA MKULIMA
					ILIYOBEBESHWA	ISIYOBEBESHWA		
1								
2								
3								
4								
5								
6								
	JUMLA							

MZALISHAJI:

Jina _____

Saini _____

Tarehe _____

Simu:_____

AFISA MTENDAJI WA KIJIJI:

Jina _____

Saini _____

Tarehe _____

Simu:_____

Mhuri.....

AFISA UGANI /KILIMO-KIJIJI/KATA

Jina _____

Saini _____

Tarehe _____

Simu:

MKURUGENZI MTENDAJI (W):

Jina _____

Saini _____

Tarehe _____

Simu:_____

Mhuri.....